**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MGENI RASMI MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA KATIKA KONGAMANO LA WIKI YA MADINI TANZANIA 2024 LINALOANDALIWA NA SHIRIKISHO LA VYAMA VYA WACHIMBAJI MADINI TANZANIA (FEMATA)

**20 JUNI 2024**

**JKICC - JIJINI DODOMA**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!...**

Napenda kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana hapa kwa ajili ya Kongamano hili la wadau wa madini nchini. Kipekee nakushukuru Mheshimiwa Anthony Peter Mavunde (Mb.), Waziri wa Madini, kwa kumwalika Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kufungua Kongamano hili. Mheshimiwa Rais alipenda kujumuika nanyi hapa leo, lakini ameshindwa kutokana na majukumu mengine ya kitaifa na amenituma nimwakilishe. Pia, napenda kuwashukuru, Rais wa Shirikisho la Vyama vya Wachimbaji Wadogo wa Madini Tanzania (FEMATA) na Viongozi wa wachimbaji wadogo wa madini kila mkoa kwa kufanikisha Kongamano hili muhimu.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Shughuli za uchimbaji mdogo wa madini ni mhimili muhimu katika maendeleo ya Sekta ya Madini nchini, ambayo inachangia takribani asilimia 40 ya mapato yatokanayo na Sekta ya Madini. Vilevile, uchimbaji mdogo wa madini una machango mkubwa katika kutoa ajira, malighafi kwa viwanda, fedha za kigeni na kuchangia mapato ambayo yanaiwezesha Serikali kuwekeza kwenye maendeleo ya nchi.

Uwekezaji unaoendelea kufanywa na sekta binafsi na Serikali katika Sekta ya Madini, umetuletea matokeo makubwa. Mathalani, mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 7.3 mwaka 2021 hadi asilimia 9.0 mwaka 2023; Vituo vya ununuzi wa madini vimeongezeka kutoka 61 mwaka 2020/21 hadi vituo 100 mwaka 2023/24; na katika kipindi kama hicho masoko ya madini yamefikia 42. Mwenendo huu unatupa matumaini kwamba Sekta ya Madini itafikia lengo la kuchangia hadi asilimia 10 kwenye Pato la Taifa kama ilivyotarajiwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Kwa ujumla shughuli za madini hasa uchimbaji mdogo, zinagusa moja kwa moja maendeleo ya watu hususani katika maeneo yenye migodi.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Naomba kuwakumbusha kuwa, mojawapo ya vigezo vinavyozingatiwa na wawekezaji na wafanyabiashara kuwekeza au kufanya biashara katika nchi yoyote duniani ni pamoja na uchumi imara, utulivu wa kisiasa (amani), sheria na sera rafiki na zinazotabirika kwa wawekezaji pamoja na uharaka wa kufanya maamuzi. Kwa ajili hiyo nakubaliana na Kauli mbinu ya Kongamano hili inayosema ***"Amani Iliyopo Tanzania Itumike Kuleta Soko la Madini Afrika Nchini Tanzania, kwa Uchumi Imara".*** Natambua kuwa Kongamano hili ni moja ya jitihada hizo za kukuza na kuitangaza Sekta ya Madini kwa kuwaleta pamoja wadau katika sekta ya madini ili kujadili fursa mbalimbali zilizopo, ikiwemo masoko; upatikanaji wa mitaji; teknolojia za uchimbaji; uchenjuaji; uongezaji thamani ya madini; na kujadili ufumbuzi wa changamoto mbalimbali zinazowakabili. Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa rasilimali zetu za madini zinatumika kimkakati na zinachangia katika kuinua uchumi na ustawi wa Watanzania wote.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Serikali imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali katika kulinda na kuendeleza rasilimali za madini hapa nchini. Baadhi ya jitihada hizo, ni pamoja na uwekezaji na maboresho katika mnyororo wa thamani, kuanzia hatua ya uchimbaji, uchenjuaji, usafishaji, uongezaji

thamani, na utoaji wa huduma mbalimbali katika shughuli za miradi ya madini. Uwekezaji na maboresho hayo unaenda sambamba na uendelezaji wa sekta fungamanishi za viwanda, ujenzi, kilimo, usafirishaji, mawasiliano na nishati. Kadhalika, Serikali inaendelea kuhamasisha na kuviwezesha viwanda vya ndani vya kuchenjua dhahabu kufanya taratibu za kupata Ithibati ya *London Bullion Market Association (LBMA)* ili kuwezesha dhahabu inayosafishwa kutambuliwa kwenye masoko ya kimataifa na kuweza kununuliwa kwa ajili ya kuhifadhiwa kama fedha.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Nchi yetu imebarikiwa na rasilimali nyingi ikiwemo za madini ya aina mbalimbali. Hata hivyo, fursa za uchimbaji madini zimeambatana na changamoto kubwa za kimazingira kwa ujumla na hususan kwa wachimbaji wadogo. Maeneo mengi nchini yameathirika kutokana na changamoto za uharibifu wa mazingira unaohusisha shughuli za uchimbaji mdogo wa madini. Athari ni kubwa na zinazidi kuongezeka katika maeneo mbalimbali ya uchimbaji hususan Geita na Chunya mkoani Mbeya. Uharibifu huo unatokana na uwepo wa mashimo yaliyotelekezwa baada ya uchimbaji wa madini, ikiwa ni pamoja na ukataji wa misitu kwa ajili ya kupanua maeneo ya uchimbaji, uharibifu na vyanzo vya maji na matumizi holela ya kemikali ya zebaki. Hali hii ya uharibifu mazingira imesababisha maeneo hayo kushindwa kutumika tena kwa shughuli za kibinadamu kama kilimo na ufugaji. Naomba nitumie fursa hii kuwaasa kuwa na uchimbaji endelevu ambao unazingatia urejeshaji wa ardhi baada ya uchimbaji ili kulinda hifadhi ya mazingira ikiwemo uoto wa asili na vyanzo vya maji na kurejeza maeneo yaliyotumika kwa uchimbaji, katika hali yake ya asili na yaweze kutumika kwa shughuli nyingine za kiuchumi.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Washiriki;***

Nimeelezwa hapa kuhusu changamoto kadhaa zinazoendelea kuwakabili wachimbaji wadogo wa madini. Nawahakikishia kuwa Serikali iko kazini na inaendelea kuweka mazingira bora katika sekta ya uchimbaji mdogo kama sehemu ya mkakati wa kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu. Naomba niyasemee machache na mengine naomba tuyachukue ili tukayatazame na kuona namna bora ya kuyapatia ufumbuzi.

***Lipo suala kwamba kodi inachangia bei kubwa ya vifaa na mitambo ya kuchimbia, kuchenjulia na teknolojia zingine***. Hili niwakumbushe viongozi wa FEMATA kwamba, kila mwaka kuanzia mwezi Disemba, Wizara ya Fedha kupitia Kamati ya Maboresho ya Sera za Kodi, huwa inatoa tangazo kwa wadau mbalimbali kutuma maoni yao hasa changamoto wanazokumbana nazo ama fursa za kodi wanazoziona. Maoni hayo hufanyiwa uchambuzi wa kina na mwishowe baada ya kuridhiwa huwasilishwa Bungeni kupitia Bajeti Kuu ya Serikali. Hivyo nawaomba viongozi wa FEMATA ifikapo mwezi Disemba kila mwaka wasilisheni changamoto hii Wizara ya Fedha ili iweze kufanyiwa kazi.

***Kuhusu kukithiri kwa tozo zinazotozwa na Halmashauri mbalimbali,*** nisisitize tu hapa kwamba, Halmashauri zote za Wilaya na Miji, ziandae sheria ndogondogo ambazo hazikinzani na Sheria ya Madini ili kuona namna bora ya kuweka tozo zenye tija. Aidha, natoa rai kwa Halmashauri zote zenye migodi, kuitumia fursa za uwepo wa migodi katika

maeneo yao na mapato yanayopatikana kama chachu ya kuleta maendeleo yenye tija kwa kizazi cha sasa na cha baadae. Vilevile, Halmashauri ziendelee kubuni miradi hasa inayowawezesha wananchi kujipatia kipato ili kuongeza mzunguko wa fedha na kuleta maendeleo endelevu kwa kuwa rasilimali madini kuna siku zitakwisha.

***Lipo suala la urasimishaji na utengaji wa maeneo ya wachimbaji wadogo***, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya marekebisho ya baadhi ya Kanuni na Sheria ya Madini na kuboresha mazingira ya biashara ya madini ikiwamo kuweka utaratibu wa kutenga maeneo ya wachimbaji wadogo ili kuwezesha wachimbaji wadogo wa madini nchini na wadau mbalimbali kushiriki ipasavyo katika uchumi wa madini. Napenda kutumia fursa hii kuwashauri wachimbaji wote, waongezaji thamani na wafanya biashara wa madini, waendelee kufuata sheria ili kuepuka usumbufu ikiwemo kufutiwa leseni zao.

***Waheshimiwa Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Ninapokaribia mwisho mwa hotuba yangu, napenda kusisitiza mambo yafuatayo:

**Jambo la Kwanza**: Wadau wote wa Sekta ya Madini hamna budi kuzingatia na kufuata Sheria na Kanuni za madini ikiwa ni pamoja na kutotorosha madini ili kuondoa usumbufu na kurahisisha utendaji wa shughuli zenu na Serikali kwa manufaa ya wote. Aidha, wachimbaji lazima mhakikishe mnakuwa mstari wa mbele katika kulipa tozo na ushuru halali ili kusaidia kuongeza mchango wa sekta ya madini katika ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

**Jambo la Pili**: Wizara ya Madini zishirikisheni Wizara manazofanya nazo kazi katika eneo la uchimbaji madini kwa mfano Wizara ya Ardhi, Maliasili na Utalii, Maji na Mazingira kabla ya kutoa leseni kwa wachimba madini ili kuepuka migogoro na muingiliano wa shughuli nyingine kulingana na matumizi bora ya ardhi kwenye maeneo husika. Mfano hapa Dodoma hapo kwenye kilima cha UDOM eneo la Njedengwa, kuna uchimbaji wa madini ya kokoto unaendelea, hali ambayo inaharibu kabisa mazingira. Mwaka juzi niliagiza kilima kile chote kipandwe miti ili kupendezesha mandhari ya pale na jiji letu. Lakini leo kuna viongozi wametoa vibali kuchimba kokoto na kifusi. Waziri wa Madini na Waziri wa Nchi Muungano na Mazingira angalieni namna bora ya kuratibu shughuli za uchimbaji madini ili kuepuka uharibifu wa mazingira katikati ya Miji na Majiji.

**Jambo la Tatu**: Bado kuna wachimbaji wengi wadogo wanafanya shughuli za uchimbaji kwa kubahatisha. Matokeo yake wanatumia muda mwingi na nguvu kubwa na kuambulia kidogo na wakati mwingine kukosa kabisa. Wizara ya Madini lazima iongeze wigo na jitahada za utafiti wa madini kupitia Taasisi ya GST ili kuwaongoza vyema wachimbaji wetu wadogo kutoka kwenye kuchimba kwa kubahatisha.

**Jambo la Nne**: Serikali imekuwa ikipoteza nguvu kazi kubwa kutokana na vifo vinavyotokea katika migodi mbalimbali. Wizara ya Madini isimamie Sheria na Kanuni za Uchimbaji bora na salama ili kuepuka ajali zisizo za lazima zinazopelekea vifo na majeraha kwa wachimbaji wadogo.

**Jambo la Tano**: kuhusu ajira na mapato tunayopoteza kutokana na kutosimamia ipasavyo utaratibu wa kuongeza thamani madini yanayopatika hapa nchini. Madini mengi bado yanaongezwa thamani nje ya nchi. Wizara ya Madini simamieni utekelezaji wa

mkakati wa kuhakikisha kwamba madini yanayochibwa yanaongezwa thamani nchini Tanzania na hivyo kusaidia kuongeza upatikanaji wa mapato na ajira kwa watanzania.

**Jambo la Sita:** Wizara ya Madini na Tume ya Madini hakikisheni wachimbaji wadogo waliopata leseni za madini na kuwekeza mitaji yao wasinyang'anywe kwa kigezo kuwa walipewa leseni hizo kwenye maeneo ya wachimbaji wakubwa. Ni suala lisiloeleweka vizuri kumpatia mchimbaji mdogo leseni ya uchimbaji madini na baada ya kuanza uwekezaji ananyang'anywa leseni hiyo na mamlaka ileile iliyompatia leseni. Hii inaleta hisia za uwezekano wa uwepo wa mazingira ya rushwa.

**Jambo la Saba:** Wizara ya Madini na Tume ya Madini angalieni uwezekano wa kuwataka wachimbaji wakubwa na wa kati wanaochimba madini yenye thamani kubwa (rare earth and strategic minerals) kurejesha mchango wao kwa jamii katika maeneo yanayowazunguka. Kwa mfano hapa Dodoma katika vijiji vya Asanje, Duluu, Gawaye na Itiso kuna uchimbaji wa madini unaoendelea lakini wananchi wa maeneo hayo hawanufaiki kabisa na chochote. Hawa wawekezaji wanachimba na kuwaachia vumbi na mashimo makubwa wakati wananchi hao hawana hata huduma muhimu za kijamii ikiwemo afya na maji. Narejea tena wakumbusheni wawekezaji hao kurejesha mchango wao kwa jamii.

***Waheshimiwa Viongozi, Ndugu Washiriki na Wananchi;***

Nawashukuru tena kwa kujitokeza kwa wingi kushiriki katika Kongamano hili muhimu. Wito wangu kwenu ni kwamba, tumieni vyema fursa hii kujifunza, kukuza mitandao yenu na kutafuta suluhisho la changamto zenu kwa pamoja. Aidha, napenda kuwaalika wawekezaji kutoka ndani na nje ya nchi kuwekeza kwenye Sekta ya Madini kwani fursa za kibiashara zipo za kutosha na Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya kazi zao kwa amani na usalama.

Mwisho kabisa, napenda kuwakumbusha nyote kushiriki kikamilifu katika kutoa maoni yenu kuhusu Dira ya Maendeleo ya Taifa 2050. Baada ya kusema hayo, napenda sasa kutamka rasmi kuwa **Kongamano la Wiki ya Madini Tanzania 2024 hapa Mkoani Dodoma** limefunguliwa rasmi.

**MUNGU IBARIKI TANZANIA!**

**ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA**